

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**  
**مَشْرُوعُ تَعَلُّمِ الْإِسْلَامِ – أَصُولُ الْعَقِيدَةِ - سَوَاحِيلِي**

**Samo la 7**

**الدرس السابع**

1- Kufuata nako ni kujisalimisha, na huko kufuata ni lililojulishwa kwenye LAAILAAHA ILLALLAH, tofauti la Kufuata na kukubalika , ni kwamba kukubalika ni kudhihirika kwa jambo na kuswihi maana yake, ama kufuata na kufuatisha jambo kwa kufanya kwa vitendo.

Yeyote atakaejua maana ya LAAILAAHA ILLALLAH akayakinisha moyoni mwake, akaikubali lakini akaacha kuifuata, akaitangaza, akajisalimisha, akaufanyia kazi muktadha wa yale aliyoyajua kwenye hii kailma ya LAAILAAHA ILLALLAH akawa wakati huo hajahakikisha sharti la kufuata, basi mtu huyo atakuwa na mapungufu kwenye kuifuata LAAILAAHA ILLALLAH.

قال الله تعالى: ﴿ وَأَنْبِئُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ ﴾ [الزمر: ٥٤]

Allah (sw) anasema (“...Na rejeeni kwa mola wenu na mjisalimishe kwake”) (Az-zumar:53).

وقال تعالى: ﴿ فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴾ [النساء: ٦٥].

Allah (sw) anasema: (“Naapa kwa nafsi yake Allah tukufu, kwamba hawatamini kikweli mpaka wakufanye wewe ni hakimu kwenye ugomvi unaotokea baina yao, kasha wasiingiwe na dhiki katika nafsi zao kwa matokea ya hukumu yako, na wajisalimishe kisawa sawa”) (Ann- Nisaa:65).

2- Ukweli na huo ukweli ni mtu kusadikisha kwenye Imani yake, kusadikisha kwenye aqeeda yake kama ambavyo anasema Allah (sw) :

قال تعالى: ﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ ﴾ [التوبة: ١١٩]

(“ Enyi mlioamini mcheni Allah na kuweni na watu wakweli”) (At-Taubah :119).

Na mtume (saw) anasema :

وقال ﷺ: (( من شهد أن لا إله إلا الله صادقاً بها دخل الجنة )) [رواه أحمد، وصححه الألباني]

(“Mwenye Kushuhudia ya kwamba hakuna mola anayepaswa kubudiwa isipokuwa ni Allah, akawa ni mwenye kusadikisha LAAILAAHA ILLALLAH ataingia peponi”) (Ameipokea Imamu Ahmad na akaisahihisha Al Bani).

Na atakapo itamka shahada kwa ulimi wake, akaikadhibisha kwenye moyo wake, basi haitamsaidia, bali ataingia na kuhesabiwa miongoni mwa watu wanafiki.

Miongoni mwa mambo yanayozuia ukweli ni kuyakadhibisha yale aliyokuja nayo bwana Mtume (saw) au kuyakadhibisha baadhi ya aliyokuja nayo mtume wa Allah, kwani Allah (sw) ametuamrisha kumtii mtume wake na kumsadikisha, akafungamanisha na kumtii yeye pale aliposema Allah (sw) :

قال تعالى: ﴿ قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ ﴾ [النور: ٥٤]

(“mtiini Allah na mumtii Mtume ”) ( An-Nur : 54).